# HALMASHAURI YA WILAYA CHALINZE

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 30/09/2021 KATIKA OFISI YA MKUU WA KITENGO CHA MANUNUZI

### WALIOHUDHURIA

1. Ndg Shabani Millao- Mkuu wa idara ya takwimu na ufuatiliaji (W) Mjumbe
2. Ndg Anne D. Mwandiga-Mkuu wa Kitengo cha manunuzi(W) –Katibu
3. Ndg John Chizima-Kaimu mkuu wa idara ujenzi (W)-Mjumbe
4. Ndg Rosemary Kamugisha-Kaimu mkuu kitengo cha sheria(W)-mjumbe
5. Dr Allen Mlekwa -Mganga mkuu wa Wilaya(W) –Mjumbe
6. Mwl Salama Ndyetabura-Mkuu wa idara ya elimu msingi (W)-Mjumbe

### SEKRETAETI

1. Julieth Kimaro- Afisa Manunuzi II
2. Jactan Kaduma-Afisa Manunuzi II

### AGENDA ZA KIKAO

1. Kufungua kikao
2. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Bodi ya zabuni cha tarehe 21/12/2021
3. Yatokanayo na kikao cha Bodi ya zabuni cha tarehe 21/12/2021
4. Kuidhinisha njia ya Manunuzi "Force Account" kwa ajili ya ujenzi wa miradi ifuatayo:
    - Ujenzi wa wodi ya wanawake na wodi ya wanaume hospitali ya Wilaya
    - Umaliziaji jengo la utawala (Pavement)
    - Ujenzi wa madarasa shule za sekondari na shule za msingi
    - Ujenzi wa zahanati (Visakasi,Kilemela na Mindutulieni)
5. Kuidhinisha njia ya manunuzi kwa ajili manunuzi ya PC 20 za taa za Barabarani kwa ajili ya stendi ya mabasi Kibiki –Chalinze
6. Mengineyo
7. Kufunga kikao.

### AGENDA I: KUFUNGUA KIKAO

Katibu alitoa taarifa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya zabuni Ndg John Mlyambate bado yupo masomoni , wajumbe wanatakiwa kuchagua Mwenyekiti wa kikao hiki

ili aongoze mjadala. Wajumbe walimchagua Ndg. Shabani Millao kuwa mwenyekiti. Baada ya kumchagua Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 5:45 asubuhi. Mwenyekiti aliwaomba wajumbe wampe ushirikiano wa kutosha kwa nasafi hiyo aliyopewa ili kufikia maamuzi yenye tija na kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao.

**AGENDA 2; KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 21/09/2021**

Katibu aliwasilisha muhtasari wa kikao kilichopita ambacho kilifanyika tarehe 21/09/2021. Kwenye muhtasari kulikua na masahihisho madogo ya mjumbe mmoja kutokuwepo kwenye orodha ya wajumbe wa kikao kilichopita. Katibu alisema atarekebisha kwenye muhtasari ambayo yalifanyika.

Mwenyekiti aliuliza kama kuna mjumbe ana hoja nyingine katika kipengele hicho wajumbe walijibu hakuna hoja mwenyekiti aliamuru katibu kuwasilisha agenda inayofuata.

**AGENDA 3: KUIDHINISHA NJIA YA MANUNUZI USHINDANI MDOGO (MINI COMPETITIVE QOTATION) KWA NYUMBA YA MTUMISHI (THREE IN ONE) NA ''FORCE ACCOUNT'' KWA AJILI YA UJENZI WA MADARASA KWA SHULE ZA SEKONDARI ,MSINGI NA UJENZI WA BWENI LA WANAFUNZI.**

Serikali inatarajia kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze **Tsh. 1,770,000,000.00 (Bilioni moja, miliono mia saba na sabini tu)** kwa ajili ya Ujenzi wa madarasa **66 (sitini na sita)** kwa shule za sekondari **14 (kumi na nne)** kwa shule shikizi za msingi, Bweni la wanafunzi na Nyumba ya Mtumishi (3in1)

Fedha hizi ni kupitia Mpango wa maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya Uviko-19

Katibu alieleza kuwa serikali ina mpango wa kuipatia Halmashauri kiasi cha 300,000,000 kwa ajili ya Ujenzi wa wodi ya wanaume na wanawake. Sambamba na fedha hizi pia serikali ina mpango wa kuipatia Halmashauri kiasi cha Tsh.150,000,000 kwa jili ya ujenzi wa zahanati ya Visakazi Kilemela na Mindutulieni

Pia katibu alieleza kuwa serikali ina mpoango wa kuipatia halm

ndani ya Halmashauri ikiwemo ujenzi wa majengo matano katika hospitali ya Wilaya na jengo la utawala.

**UJENZI WA MADARASA THEMANINI YA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KITENGO CHA MANUNUZI KILIPENDEKEZA YAFUATAYO:**

Katibu alieleza kuwa katika ununuzi wa vifaa baadhi ya mahitaji yatanunuliwa katika vituo husika ngazi ya msingi Sababu ya msingi ya kugawa vifaa hivi katika maeneo husika ni kuwa mahitaji haya yanapatikana kwa urahisi na bei nafuu katika maeneo husika .

Katibu alieleza kuwa vifaa vingine vitanunuliwa kwa pamoja na Halmashauri . Manunuzi ya pamoja yataunganishwa na kisha kununua kwa watengezaji , mawakala wakubwa na wafanyabiashara wakubwa wanaoweza kutoa punguzo kubwa la bei. . Lengo kubwa hapa ni kuokoa fedha na kusaidia upatikanaji wa vifaa kwa wakati na vifaa vinavyofanana ubora.Vifaa vinavyopendekezwa kununuliwa katika ngazi ya msingi ni vifuatavyo:

1. Kokoto
2. Mchanga
3. Mawe
4. Tofali
5. Mafundi
6. Mbao za kujengea box

Katibu alieleza kuwa vifaa vinavyopendekezwa kununuliwa kwa mfumo wa manunuzi ya pamoja ni vifuatavyo:

1. Nondo mm 12 nondo 6mm
2. Saruji
3. Mbao za kupaulia
4. Misumari ya kupaulia na misumari ya kuezekea
5. Bati na kofia

Katibu alieleza
kuwa katika utekelezaji wa "force account" njia za manunuzi zinazopendekezwa kutumika ni zifuatazo:

1. Ushindanishi mdogo "Competitive Quotations"
2. Chanzo kimoja "Single Source"

Pamoja na taarifa yake katibu iliomba kuwa kwa utaratibu huu endapo bodi ya zabuni itaridhia mapendekezo haya aliiomba Bodi ya zabuni kuidhinisha orodha ya wazabuni ambao watatumika kutoa huduma ya kusambaza vifaa vya ujenzi. Wazabuni walipendekezawa ni wafuatao:

| S/NO | JINA LA MZABUNI | AINA YA VIFAA |
|---|---|---|
| 1. | M/S JUGOJ ENTERPRISES P.O.BOX 13 CHALINZE | VIGAE VYA SAKAFU "TILES" |
| 2. | M/S KAZALIWA &COMPANY LTD P.O.BOX 16647 CHALINZE | VIFAA MCHANGANYIKO |
| 3. | M/S ABINIEL TIMOTH MGOBA P.O.BOX 425 MOROGORO | VIFAA MCHANGANYIKO |
| 6. | M/S MWAMBI ENTERPRISE P.O.BOX 40937 DAR ES SALAAM | MBAO NA VIFAA MCHANGANYIKO |
| 7. | M/S VGK COMPANY LIMITED P.O.BOX 66608 DAR ES SALAAM | SARUJI NA KOKOTO |
| 8 | DANGOTE CEMENT LIMITED TANZANIA P.O.BOX 1241 MTWARA | SARUJI |
| 9. | KIBOKO PAINTS (T) LTD P.O.BOX 3030 DAR ES SALAAM | RANGI |
| 10. | MM INTERGRATED STEEL MILLS LTD P.O.BOX 3030 DAR ES SALAAM | BATI,NONDO,MISUMARI YA BATI NA YA KUJENGEA |
| 11 | M/S AYISEWA LIMITED P.O.BOX 61414 DAR ES SALAAM | MADAWATI |
| 12. | M/S BONELE TRADING BOX 46 CHALINZE | MADAWATI |
| 13. | M/S BHURUHANI FURNITURE AND BUILDING PRODUCTS COMPANY P.O.BOX 941 TANGA | MADAWATI |

Wajumbe walipokea maelezo ya katibu na walilidhia mapendekezo ya kitengo cha manunuzi . Wajumbe walihohji kuhusu mfumo wa malipo ,hoja hii ilichangiwa na wajumbe mablimbali ambapo ilifikwa muafaka kuwa wakuu wa shule wataitwa katika kikao kupewa maamuzi haya ili kuwa nauelwa aw pamoja. Sambamba na hilo afusa masuuli pamoja mna mwekahazina wawasilsihiwe ushauri wa kukusnya fedha katika akaunti ya amana ili zikusnaywe na kulipa kwa pamoja kwa wazabuni wtakaopitishwa. Aidha mkuu wa kitengo cha manunuzi alieleza kuwa mfumo huu hauna tofauti na mfumo wa manunuzi ya pamoja kwa wakalala wa unuzi gpsa tunaponunua magari na mafuta nafiafaa vingine hivyo ni utaratibu ambao upo na unatumikaBodi ya zabuni ilimpa katibu agizo la kuwasilisha taarifa kwa afisa masuuli ili taratibu zinazofuata ziendelee.

**WAZABUNI WALIOIDHINSHWA NA BODI YA ZABUNI KUSHINDANISHWA KWA AJILI YA UJENZI "PAVEMENT" NA WODI YA WANAWAKE NA WADI YA WATOT0**

| S/NO | JINA LA MZABUNI | AINA YA VIFAA |
|---|---|---|
| 1. | M/S JUGOJ ENTERPRISES P.O.BOX 13 CHALINZE | VIGAE VYA SAKAFU "TILES" |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | M/S KAZALIWA &COMPANY LTD P.O.BOX 16647 CHALINZE | VIFAA MCHANGANYIKO |
| 3. | M/S ABINIEL TIMOTH MGOBA P.O.BOX 425 MOROGORO | VIFAA MCHANGANYIKO |
| 4. | M/S SODOX TRADING &SERVICES LTD P.O.BOX 77162 DAR ES SALAAM | MADIRISHA YA CHUMA NA VIOO |
| 5. | M/S INSIGNIA LTD P.O.BOX 71449 DAR ES SALAAM | RANGI |
| 6. | M/S MWAMBI ENTERPRISE P.O.BOX 40937 DAR ES SALAAM | MBAO |
| 7. | M/S VGK COMPANY LIMITED P.O.BOX 66608 DAR ES SALAAM | SARUJI NA KOKOTO |
| 8. | M/S DANGOTE CEMENT LIMITED TANZANIA P.O.BOX 1241 MTWARA | SARUJI |
| 9 | M/S JINQIAO COMPANY LTD P.O.BOX 517 DAR ES SALAAM | TOFALI ZA SAKAFU |
| 10 | M/S INSIGINIA LTD P.O.BOX 71449 DAR ES SALAAM | RANGI |
| 11. | M/S HASSAN MOHAMEDY RASHIDY P.O.BOX 65 CHALINZE | MAWE |
| 12 | M/S AYISEWA LIMITED P.O.BOX 61414 DAR ES SALAAM | MILANGO |
| 13. | M/S MAWEGU ENTERPRISES P.O.BOX 45412 DAR ES SALAAM | TOFALI ZA ASAKAFU NA VIFAA VYA UJENZI WA SAKAFU |
| 14. | M/S MIRAJI SUFIANI OMARY P.O.BOX 48 CHALINZE | VIFAA MCHANGANYIKO |
| 15 | M/S KASOME SUPPLY P.O.BOX MLANDIZI | VIFAA MCHANGANYIKO |
| 16 | M/S ANDREA HARDWARE P.O.BOX CHALINZE | VIFAA MCHANGANYIKO |
| 17. | M/S BHURUHANI FURNITURE AND BUILDING PRODUCTS COMPANY P.O.BOX 941 TANGA | MILANGO YA MBAO |

Wajumbe walipokea maelezo ya katibu na walilidhia mapendekezo ya kitengo cha manunuzi. Bodi ya zabuni iligiza utaratibu unaofuta uendelee.

**AGENDA 5: KUIDHINISHA MANUNUZI YA PC 20 ZA TAA ZA BARABARANI**

Katibu alitoa taarifa kuwa amepokea maelekezo ya kufanya manunuzi ya taa za barabarani PC 20 kwa ajili ya stendi ya mabasi Kibiki inayoendelea kujengwa . Kitengo cha manunuzi kinapendekeza njia ya chanzo kimoja "Single source", kwa kumtumia mzabuni BONWAY INTERNATIONAL ambaye alifanya kazi ya kuweka taa za barabarani katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021. Sababu za mapendekezo ya njia na mzabuni ni zifuatazo:

1. Katika kazi aliyofanya katika mwaka wa fedha 2020/2021 katika ununuzi wa PC 80 katika uwekaji wa taa katika maeneo ya barabara za Chalinze Msata na Lugoba hakuna hitilafu iliyotokea mpaka sasa ambapo
2. Ubora wa bidhaa na kipindi kirefu cha matazamio

**AGENDA 6: MENGINEYO**

Hakukuwa na mengineyo yaliyopokelewa na Mwenyekiti.

**AGENDA 8: KUFUNGA KIKAO**

M/kiti alifunga kikao mnamo saa 6:30 mchana. aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na aliwaomba kutoa ushirikiano wa kutosha kwa vikao vinavyofuata
.

**MHUTASARI UMETHIBITISHWA NA:**

.................................. 8/10/2021 .................................. ..................................